



>>> Orientation to Ontario

MANUFAA NA MSAADA WA KIJAMII

MANUFAA

Bima ya Ajira (EI)

Unaweza kustahiki manufaa ya Bima ya Ajira (EI) ikiwa utapoteza kazi yako kwa sababu zilizo nje ya uwezo wako, kama vile uhaba wa kazi, au kuachishwa kazi kwa msimu au kwa wingi. Ili kustahiki EI, lazima uwe umefanya kazi kwa saa za kutosha zisizoweza kulipiwa bima nchini Kanada katika wiki 52 zilizopita.

Ili kujua zaidi kuhusu EI, tembelea Service Canada (Huduma Kanada) kwa servicecanada.gc.ca or findlink.at/cpp

Canada Pension Plan (Mpango wa Bima Kanada) (CPP)

Unapokuwa na umri wa miaka 65 unaweza kuhitimu kupokea malipo ya uzeeni ya kustaafu ya CPP. Ni lazima utoe mchango angalau mmoja kwa mpango wakati wa maisha yako ya kazi nchini Kanada. Unaweza kuchukua CPP (Mpango wa Bima Kanada) yako kati ya umri wa miaka 60 na 64, lakini malipo yako yatapunguzwa. Ukielewesha kukusanya manufaa yako ya CPP (Mpango wa Bima Kanada), malipo yako yanaweza kuongezeka.

Ili kujua zaidi kuhusu CPP (Mpango wa Bima Kanada), tembelea Service Canada (Huduma ya Kanada) kwa findlink.at/cpp

Old Age Security Pension (Pensheni ya Usalama wa Wazee) (OAS)

Haya ni mafao ya kila mwezi yanayolipwa kwa Wakanada walio na umri wa miaka 65 au zaidi. Ili kuhitimu, lazima uwe umeishi Kanada kwa angalau miaka 10 baada ya kufikisha miaka 18.

Ili kujua zaidi kuhusu OAS (Pensheni ya Usalama wa Wazee), tembelea Service Canada (Huduma ya Kanada) kwa findlink.at/oldagesecu

Canada Child Benefit (CCB) (Mafao ya Canada kwa Mtoto)

CCB (Mafao ya Kanada kwa Mtoto) ni malipo ya kila mwezi kutoka kwa serikali ya jimbo ili kusaidia wazazi na walezi wengine na gharama ya kulea watoto. Lazima uwasilishe maombi ya mafao. Kima cha mafao ubadilishwa kulingana na kiwango cha mapato.

Ili kujua zaidi kuhusu CCB (Mafao ya Kanada kwa Mtoto), tembelea Canada Revenue Agency (Shirika la Ukusanyaji Ushuru la Kanada) kwenye canada.ca au findlink.at/cra-bnfts

Ontario Child Benefit (OCB) (Faida za Mtoto wa Ontario)

OCB (Faida za Mtoto wa Ontario), malipo ya kila mwezi kutoka kwa serikali ya jimbo kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka sita. Mafao yanatolewa kwa familia ili kusaidia gharama ya kulea

Funded by / Financé par :



Immigration, Refugees
and Citizenship Canada

Immigration, Réfugiés
et Citoyenneté Canada

mtoto. Mafao ni kwa familia zote, sio tu kwa wale wanatumia huduma za kulea watoto.

Ili kujifunza zaidi kuhusu OCB ((Faida za Mtoto wa Ontario), tembelea Service Canada (Huduma Kanada) kwenye findlink.at/UChildCB

MSAADA WA KIJAMII

Ontario Works (OW) (Kazi za Ontario)

Mpango wa Ontario Works (Kazi za Ontario) inatoa msaada wa kifedha kwa watu walio na mahitaji ya muda ya kifedha. Mpango huu pia hutoa msaada kwa ajili ya kutafuta kazi.

Ili kujua zaidi kuhusu OW (Kazi za Ontario), tembelea Wizara ya Watoto, Jamii na Huduma za Jamii kwa ontario.ca

Mpango wa Msaada wa Walemvu wa Ontario (ODSP)

Mpangohuu husaidia watu wenye ulemavu ambao wana mahitaji ya kifedha. ODSP pia inasaidia watu wenye ulemavu ambao wanaweza kufanya kazi kupata kazi.

Ili kujua zaidi kuhusu ODSP (Kazi za Ontario), tembelea Wizara ya Watoto, Jamii na Huduma za Jamii kwa findlink.at/Ont-DSP

JE, UNAJUA?

Umri ambao OAS huanza unabadiika polepole. Watu waliozaliwa mwaka wa 1958 na baadaye wataathiriwa na mabadiliko haya, kwani umri wa kustahiki utaongezeka.

